BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 29 Juni, 2018.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Mahakama, Kufafanua Utumishi wa Mahakama, Kuanzisha Ofisi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Mrajis, Kuanzisha Mfuko wa Mahakama, na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusina na Hayo.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na Kuweka Masharti ya Ukaguzi wa Elimu Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusina na Hayo.

Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar na kuweka masharti bora yanayohusiana na Kazi, Uwezo, Uongozi na Mambo Mengine Yanayohusina na Hayo.

III. MASWALI:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

106. MHESHIMIWA HIDAYA ALI MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hivi karibuni kumetokea mkanganyiko kwa baadhi ya wanafunzi wanaotoka kidato cha nne kwenda kidato cha sita ambao wamepata matokeo yao ya Mtihani wa Taifa 2017/18 na kuonekana kuwa wamepasi. Hata hivyo baadhi ya wanafunzi hao ambao matokeo yanaonesha wamepasi, Wizara haitambuwi pasi hizo na badala yake wamekosa nafasi za kujiunga kidato cha sita.

(a) Wizara inaweza kueleza utaratibu wa pasi na kombi za kujiunga kidato cha sita.

(b) Je, ni kwa kiasi gani vijana hao ambao pasi zao hazitambuliwi hawajakidhi vigezo hivyo.

(c) Wizara inawasaidia vipi vijana ili waweze kuendelea na masomo endapo itaonekana kuna makoseo yamefanyika kwa kuzitoa pasi zao.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

185. MHESHIMIWA ASHA ABDALLA MUSSA (Jimbo la Kiwengwa) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa muda mrefu wakulima wa mwani wamekuwa wakilalamikia bei ndogo ya zao hilo kulinganisha na kazi kubwa wanayoifanya katika kilimo hicho.

Je, Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imejipanga vipi kuhakikisha kuwa zao hilo linapanda bei na kuwafanya wakulima kufaidika na kilimo hicho.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

87. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Serikali inaendelea kufanya jitihada kubwa kukuza miundombinu ya barabara Unguja na Pemba, lakini kumejitokeza ajali za mara kwa mara katika daraja la Kitope.

Je, Serikali ina mpango gani wa kulitengeneza daraja hilo kwa haraka ili kuepusha ajali katika eneo hilo.

249. MHESHIMIWA ALI KHAMIS BAKAR (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kununua magari ya Uokozi katika kiwanja cha ndege cha A.A.Karume ili kutoa huduma bora na kwa kuwa magari haya yamenunuliwa kwa gharama kubwa na yanahifadhiwa bila ya kuwekwa katika maegesho maalum hali inayosababisha magari hayo kuharibika.

(a) Je, ni lini yatajengewa sehemu ya maegesho ili yasipigwe na jua na mvua.

(b) Ni kiasi gani cha fedha kinachohitajika katika ujenzi wa banda hilo.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

25. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

. Wizara ya Biashara na Viwanda kupitia Shirika lake la ZSTC katika matarajio yake ya mwaka 2017/2018 ni kuwapatia zawadi wakulima na wauzaji bora wa karafuu.

(a) Je, Waziri ahadi hiyo unaifahamu.

(b) Je, umechukua hatua gani ya kuitekeleza.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nyumba na Nishati:

147. MHESHIMIWA SIMAI MOH'D SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

(a) Je, ni pampu ngapi za maji zilizotolewa na Ras El Khaima zimetumika.

(b) Je, ni pampu ngapi zimebakia katika hizo na je, maeneo yaliotumika ndio yale yaliyochimbwa visima na kampuni hiyo.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Mahakama, Kufafanua Utumishi wa Mahakama, Kuanzisha Ofisi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Mrajis, Kuanzisha Mfuko wa Mahakama, na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusina na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na Kuweka Masharti ya Ukaguzi wa Elimu Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusina na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar na kuweka masharti bora yanayohusiana na Kazi, Uwezo, Uongozi na Mambo Mengine Yanayohusina na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Zanzibar,
29 Juni, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.